**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)



***Mkurugenzi Mkuu wa TCRA- Dkt. Jabiri Bakari***

***"Kuimarisha Ushirikishwaji wa Kiuchumi kupitia TEHAMA."***

**Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dkt. Jabiri Kuwe Bakari, katika kuadhimisha Siku ya Shirika la Mawasiliano Afrika (ATU), tarehe 7 Desemba 2022.**

Leo, Desemba 7, 2022, Shirika la Mawasiliano barani Afrika (ATU) linaadhimisha miaka 45 tangu lilipoasisiwa. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inashiriki katika hafla hii muhimu, inayoongozwa na kaulimbiu isemayo "Kuimarisha Ushirikishwaji wa Kiuchumi kupitia TEHAMA."

Mazingira ya ushindani yamewezesha kuchipuka kwa huduma za ziada za mifumo ya Mawasiliano, na teknolojia zinazoambatana nayo, iliyowezesha jamii, Taasisi na Serikali kuhudumiwa ipasavyo.

TCRA, ambayo inasimamia maendeleo na matumizi ya teknolojia za mawasiliano na huduma nyingine zinazohusiana na TEHAMA nchini Tanzania, imehakikisha kuwa miundombinu ya mawasiliano inasaidia ukuaji wa uchumi shirikishi. Hivyo, sekta za afya, ujasiriamali, kilimo, ubunifu, teknolojia ya kidijitali, elimu, biashara ya kimataifa, uchukuzi na nyingine nyingi zimeendelea kukua kwa kasi inayochagiza ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Ushahidi wa ukuaji huo ni jinsi watu wanavyotumia kwa manufaa huduma za kifedha za kidijitali kwa njia ya simu ya kiganjani.

Kama msimamizi wa sekta ya mawasiliano nchini Tanzania, TCRA inapenda kuwasilisha hakikisho lake kwa Menejimenti yote ya ATU juu ya ushirikiano wake wa kudumu na uliomakinika ambao kwa hakika utawezesha ATU kufikia malengo yake

katika kuhakikisha sekta ya TEHAMA katika bara letu la Afrika inakwea ngazi na kufikia upeo wa ukuaji uliotarajiwa.

Ikumbukwe kuwa katika ulimwengu wa TEHAMA, si jambo la maana kwa mataifa kujifungia, TEHAMA inahitaji mataifa kujitokeza na kuungana, kuunganisha na kufanya kazi kwa pamoja, na hiyo ndiyo sababu ya TCRA kama mwakilishi wa Tanzania katika mashirika ya Mawasiliano kikanda na kimataifa kuendelea kuwa mwanachama hai anaechangia mageuzi ya sekta katika bara la Afrika naam na kwingineko duniani.

TEHAMA ni tasnia inayohitaji ujumuishaji wa teknolojia, rasilimali, ujuzi, taratibu na viwango vya kimataifa vinavyovuka mipaka. Hayo yote lazima yafanywe kwa kuzingatia ubora na nchi na Taasisi za usimamizi wa sekta zinapaswa kushirikishana miundo bora zaidi ya usimamizi wa sekta kwa kuzingatia miongozo ya karibu inayotolewa na mashirika ya kikanda na kimataifa yanayosimamia sekta ya Mawasiliano.

Mchango wa TCRA katika kukuza uchumi jumuishi unadhihirika katika zoezi la usajili wa laini za simu za mkononi ambapo wananchi wanahakikishiwa zoezi hilo la usajili linajumuisha upatikanaji na ufikiwaji wa huduma za kifedha kwa njia ya simu.

Mathalani, hadi kufikia Septemba 2022, Tanzania ilikuwa na laini za simu zilizosajiliwa milioni 58.1 kutoka kwa wakazi milioni 61.7 kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya mwaka 2022. Hili ni ongezeko la asilimia 3.4 ya laini zilizosajiliwa ikilinganishwa na waliojisajili milioni 56.2 mwezi Juni 2022. Usajili wa watumiaji wa huduma za kifedha kwa njia ya simu unaonyesha Tanzania kuwa na watumiaji milioni 39.6 ambayo ni asilimia 68.16 ya jumla ya laini za simu zilizo kwenye matumizi.

Mamlaka ya Mawasiliano inatambua kuwa, teknolojia inakua kwa kasi sana na kuenea kwa huduma tofauti ambazo hutumiwa na watumiaji wa mwisho wa huduma za mawasiliano. Ili wananchi wote wanufaike na ukuaji huu wa teknolojia na huduma zinazohusiana, ipo haja ya upanuzi wa huduma hizo hadi maeneo ambayo hayajahudumiwa na yenye upungufu wa miundombinu na rasilimali husika ili kurahisisha utoaji wa huduma hizo zikiwemo huduma za kifedha kwa kutumia huduma za fedha kwa njia simu. Katika kufanikisha hili TCRA tunafanya kazi kwa karibu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Watoa Huduma za Mawasiliano na wadau wengine ili kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu ya mawasiliano ya mtandao katika maeneo ambayo hayajahudumiwa ipasavyo na ambayo hayajafikiwa kabisa na huduma. Hatua hii inaziba pengo linaloonekana la upatikanaji wa huduma kwa jamii yote ya waishio mijini na vijijini.

Pia, TCRA inatoa rasilimali-namba na masafa ya Mawasiliano kwa wenye leseni na watoa huduma wapya ili kuwezesha utoaji wa huduma za Mawasiliano zikiwemo huduma za kifedha. Mathalani, tarehe 11 Oktoba 2022, TCRA ilifanikiwa kunadi masafa ya Mawasiliano katika bendi mbalimbali za IMT katika vitalu vya 700 MHz, 2300 MHz, 2600 MHz na 3500 MHz.

Vitalu hivi vipya vya masafa vilivyotolewa kwa njia ya Mnada kwa watoa huduma za Mawasiliano vitaboresha na kupanua utoaji huduma hasa kwa kutumia teknolojia ya 5G. TCRA imejidhatiti kuhakikisha inaweka mazingira wezeshi yanayoruhusu Watoa

Huduma kuweza kutoa huduma zenye kukidhi viwango vya ubora wa Mawasiliano vya kitaifa na kimataifa.

TCRA inatarajia kuwa, mnada huo uliowezesha watoa huduma kuongeza wigo wa utoaji huduma utarahisisha upanuzi wa mtandao na huduma za wenye leseni zitakuwa zienye ubora zaidi hatimae kuwafikishia wananchi wengi zaidi huduma huduma za kifedha kwa njia ya simu ili kuziba pengo la ukosefu wa huduma za kibenki.

Huduma za Kifedha Kidijitali zinazidi kuwa jukwaa linalopatikana kila mahali na kwa gharama nafuu zikiongeza viwango vya ujumuishaji wa kifedha kwa kuwezesha upatikanaji wa huduma za msingi za kifedha kwa bei nafuu na kwa urahisi hasa kwa wananchi wasiofikiwa. TCRA itaendelea kuhakikisha huduma za Mawasiliano zinasimamiwa vilivyo ili kuwezesha Mawasiliano ya uhakika na kuchagiza ukuzaji wa uchumi jumuishi kwa njia ya vifaa na huduma za Mawasiliano.

Hongera ATU!

**MWISHO**